

UFALME
WAKO
UJE

# NOVENA

## Toka Kupaa hadi Pentekoste


Bishop
Anthony
Poggo

KATIBU MKUU WA KANISA
LA ANGLIKANA

UFALME WAKO UJE

# NOVENA

Ufalme Wako Uje: Novena (Kimeandikwa na Askofu Anthony Poggo)
Hakimiliki © 2024 Ufalme Wako Uje. Kimetumika kwa ruhusa. Haki zote zimehifadhiwa duniani kote.

Maandiko yaliyorejewa yametoka katika Mapitio ya Toleo Jipya la Biblia, Hakimiliki © 1989 na Kitengo cha Elimu ya Kikristo cha Baraza la Taifa la Makanisa ya Marekani. Imetumika kwa ruhusa. Haki Zote Zimehifadhiwa.

Picha zimetumika kwa ruhusa.

UFALME WAKO UJE

# NOVENA

Bishop Anthony Poggo

KATIBU MKUU WA KANISA LA ANGLIKANA

# UTANGULIZI

*'Roho Mtakatifu Uje.'* Sala hii fupi, na rahisi ndiyo kitovu cha kitabu hiki cha Ufalme Wako Uje. Kuna wimbi kubwa la sala hii ambalo limeenea katika nchi zaidi ya 172 ulimwenguni kote, chanzo chake ni kutokana na matendo ya kanisa la kwanza walipotii amri ya Yesu ya kusubiri kujazwa na Roho Mtakatifu.

Matendo ya Mitume 1:14 inatuambia kwamba msingi wa mipango yao ilikuwa ni kudumu katika maombi:

> *Wote waliungana kwa moyo mmoja katika kufanya maombi mara kwa mara, pamoja nao wanawake, na Mariamu mama yake Yesu, na ndugu zake.*

Jumuiya mpya ilizaliwa baada ya kifo na ufufuo wa Bwana Yesu. Walipewa kazi moja tu: kuwa Mashahidi wa Kristo hata mwisho wa dunia. Pentekoste ilionyesha kwamba, mpango wa Mungu wa wokovu haukuwa na kizuizi chochote cha lugha au tamaduni; kila mtu ni lazima asikie Habari Njema ya msamaha na uzima wa milele katika lugha yake mama, lugha ambayo anaielewa. Sio lazima ajifunze lugha ya kanisa; lakini, kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, kanisa lilitumwa kujifunza na kusambaza ujumbe wa Kristo kwa lugha ambayo ulimwengu ungeielewa.

Uwezo wa kitabu cha *Ufalme Wako Uje* kufikia mataifa mengi umefanya kipate nafasi maalumu Novena mwaka huu. Tunamshukuru sana Askofu Anthony Poggo, Katibu Mkuu wa Kanisa la Anglikana, kwa kuchukua jukumu la kuwa mwandishi wa mwaka huu. Ufahamu wake mkubwa juu ya Afrika, pamoja na uwezo wake wa kufanya kila bara analoenda kuwa nyumbani, utatusaidia sote kusali sala ya *'Ufalme Wako Uje'* popote pale Mungu atakapotuweka ulimwenguni.

Mwaka huu tutajikita kwenye sura za mwanzo za Ufunuo katika masomo yetu ya kila siku. Ulimwengu huu wa matatizo una mambo mengi yanayofanana na ule wa kwenye kitabu cha mwisho cha Biblia. Vurugu, ukandamizaji, unyanyasaji wa wanawake na watoto vilikuwa ni sehemu ya kawaida katika Milki ya Roma kama ilivyo ulimwenguni kote hivi leo.

Tunauinua ulimwengu huu wa Mungu kwake katika maombi yetu na kisha tunaelekeza maombi yetu kwa watu binafsi huku kila mmoja wetu akifikira watu watano anaowafahamu ambao hawamfuati Bwana Yesu. Tunasali kwamba waje na kufurahia amani yake, upendo wake na uzima wa milele unaopatikana kwake tu.

Wakristo mara nyingi wanashindwa kutimiza Agizo Kuu kwa sababu ya kuchanganywa na kuzingatia zaidi mambo ambayo yanatupishanisha sisi kwa sisi. Tunatumaini kwamba mwaka huu kitabu cha Ufalme Wako Uje kitatuunganisha pamoja katika ukweli wa Habari Njema ya Yesu na jukumu la kupeleka habari hiyo kwa wote duniani kote.

Tunatumaini kwamba utaungana na sisi katika kuomba *'Roho Mtakatifu Uje.'*

*Askofu Mkuu wa Canterbury, Justin Welby*
*Askofu Mkuu wa York, Stephen Cottrell*

1

2

3

4

5

# SIKU YA KUPAA

## Yesu ni Bwana

Ufunuo 1:4-5

*Neema na iwe kwenu na amani, zitokazo kwake yeye aliyeko na aliyekuwako na atakayekuja; na zitokazo kwa roho saba walioko mbele ya kiti chake cha enzi, tena zitokazo kwa Yesu Kristo, shahidi aliye mwaminifu, mzaliwa wa kwanza wa waliokufa, na mkuu wa wafalme wa dunia.*

*'Hivi kuna mtu huko?'*
Hakuna mtu anayepokea simu.
Hakuna jibu mlango unapogongwa.
Ujumbe mfupi wa simu haupatiwi majibu.
Sauti za ngoma zinasikika lakini hakuna mtu anayejitokeza.

*'Hivi kuna mtu huko?'* Katika ulimwengu ambao umejaa hasira na vurugu nyingi, mateso na ukosefu wa haki, kutengana na upweke na sehemu nyingi wanawake wananyanyaswa, na watoto yatima wanateswa; ni kawaida, tunapokusanyika na kusali tukiuliza swali, 'Hivi kuna mtu huko?'

Ukweli ni kwamba athari zinazotokana na uovu hazijabadilika sana tangu kipindi cha Yohana, akiwa mafichoni katika kisiwa cha Ugiriki cha Patmos, alipopata maono ya kitabu cha Ufunuo. Kwa sasa magaidi wamechukua nafasi ya majeshi ya Warumi; uvamizi na utekaji wa watu vijijini, vifo na uharibifu bado ni vile vile. Silaha zimebadilika lakini ukatili wa waovu ni ule ule.

Hivyo, ni jukumu letu, kama ilivyokuwa kwa Wakristo wa moja ya jimbo la Asia (ilipo Uturuki leo) kuyatoa maneno haya. Si tu maneno kutoka kwa Mtume aliyekuwa mafichoni bali ni maneno kutoka katika kiti cha ufalme wa mbinguni. Kuna habari njema.

Kuna mtu yupo!



*Baraza la Mashauriano la Kanisa la Anglikana, Ghana*

Huo ndio uhakikisho mkuu katika mstari wa leo. Baadhi ya Wakristo ambao Yohana aliwaandikia walikutana na mateso, kufungwa, na hata kifo sababu ya imani yao kwa Yesu. Walijaribiwa kutaka kukata tamaa kwa sababu kuwa Mkristo ilikuwa ni kinyume sana na tamaduni za wakati huo.

Yule ambaye yupo upande wa pili: Mungu Mwenyezi, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, anazungumza na watu wake maneno ya neema na amani, kuwatia moyo na kuwapa changamoto, faraja na kuwarekebisha. Ni Yesu yule yule asiyebadilika, 'ni yeye yule jana na leo na hata milele' (Waebrania 13:8).

Kuna usemi wa Kiafrika unaosema kwamba, 'Tai huwa na ujasiri wa kuchukua kifaranga cha kuku tu, mtoto wa simba hana wasiwasi', Mtoto wa simba hana haja ya kuwa na hofu ya tai kwa sababu tai anamuogopa baba yake simba. Kama tukikumbuka sisi ni nani 'ndani ya Kristo', tutapata ujasiri wa kuishinda hofu.

Kama Yohana alivyoona 'mbingu ikifunguka' jambo la faraja ni kwamba tunajibiwa na Mungu aliyetuumba sisi na vitu vyote. Bwana aliyetupa maisha yetu, akafa badala yetu na kufufuka kwa ushindi dhidi ya kifo, Roho Mtakatifu ambaye Yesu aliahidi kwa wote wanaomwamini.

**Katika siku hizi zijazo, wafikirie watu watano ambao wapo ndani ya moyo wako na ambao unaweza kuwa ukiomba juu yao tunapokuwa tunaendelea na safari hii pamoja. Tunapowaombea watu hawa watano leo, tunawaweka mbele ya Mungu wa ajabu anayewafahamu na kuwapenda. Katika upendo wake na mapenzi yake kuna amani ya milele.**

# MUNGU ANAYEPENDA

Ufunuo 1:5-6

*Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake, na kutufanya kuwa ufalme, na makuhani kwa Mungu, naye ni Baba yake; utukufu na ukuu una Yeye hata milele na milele. Amina*

Kitabu hiki cha Ufunuo kinatupa changamoto kadhaa kuhusu namna tunavyoishi na Yesu ndani ya ulimwengu ambao haujakamilika. Ukweli mzuri ni kwamba neno hili ni kwa ajili yetu, linaanza kwa kumtambulisha Bwana Yesu kwetu na ukweli huu unatupa amani katika mioyo na akili zetu: 'Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu.' Ni muunganiko wa ajabu – upendo na uhuru. Mungu anataka tufahamu kwamba ndani ya Yesu Kristo tunapendwa na tumewekwa huru. Kila mtu mmoja mmoja anapendwa, kama mhubiri mmoja alivyowahi kusema: 'Kana kwamba hakuna mwingine wa kupenda.'

Ni rahisi sana kujihisi kuwa mdogo na usiye na thamani yoyote katika ulimwengu wa leo. Matatizo ya mabadiliko ya hali ya hewa, njaa, ukosefu wa makazi, vita, kuvunjika kwa familia – yote ambayo mara nyingi huathiri masikini zaidi – yanaonekana kuwa matatizo makubwa sana.

Je, Mungu anawezaje kutupenda mtu mmoja mmoja? Anatupenda.

Biblia inatuambia ukweli huu tena na tena; lakini kama unakumbuka hadithi za injili, basi kumbuka hadithi ya yule mwanamke ambaye alitaka kuponywa na akagusa nguo ya Yesu. Hakika aliponywa; lakini Yesu, ambaye alikuwa akielekea kumsaidia binti mdogo, alisimamisha umati wa watu na kuhakikisha mwanamke yule aliyeponywa kwa kumgusa anaokolewa imani yake na kuuona uzima wa milele. (Marko 5:24-34). Licha ya umati mkubwa kumhitaji, bado Yesu alikuwa na muda wa kusimama kwa ajili ya mwanamke yule. Je, tupo tayari kwa kiasi gani kujibu wito wa Mungu wa kuwafundisha watu wengine, licha ya kuwa na ratiba zilizotubana sana?

Baadhi ya jamii huwa zinawaheshimu sana wazee na kutojali mahitaji ya vijana. Huku jamii zingine zikiwekeza katika fursa za vijana na kutowathamini wale waliofanya

kazi maisha yao yote na sasa wakiwa wanahitaji msaada. Mungu anatupenda bila kujali umri wetu, asili yetu, uraia, kabila, jinsia, elimu, kazi, utajiri, au hadhi yetu. 'Mungu ni pendo' ni moja ya misingi rahisi na bora zaidi ya kutuwezesha kufahamu namna ya kumtazama Mungu, ulimwengu na kujitazama sisi wenyewe.

Ni kweli, maneno yanaweza yakawa ni rahisi na wakati mwingine yasiwe na maana. Msemo mmoja kutoka Senegal unasema hivi: 'Anaweza kusema anakupenda; subiri uone anachokutendea.' Ndiyo maana maneno yanayofuata baada ya kutuhakikishia kwamba Mungu ni pendo yamejaa nguvu kubwa. 'Katuosha dhambi zetu katika damu yake'. Rangi ya damu ya binadamu ni moja bila kujali rangi ya ngozi yake au uraia wake. Damu iliyomwagika msalabani ni kwa ajili ya ulimwengu wote, na inaashiria nguvu ya kazi ya ukombozi ya Kristo kwa watu wote wa Mungu, bila kujali rangi yao au uraia wao.

Mwishoni mwa kitabu cha Ufunuo, upendo wa Mungu kwa kila mmoja wetu, tulioumbwa kwa sura yake, na kukombolewa kwa kifo na ufufo wa Kristo, unaonekana kwa ya kipekee sana. Tunasoma kwamba: 'Atafuta machozi yote machoni mwao.' Ili mtu akufute machozi ni lazima umruhusu akusogelee karibu.

**Unapoendelea kuomba kwa ajili ya watu wako watano leo, waweke katika uwepo wa Mungu, na omba kwamba licha ya changamoto ambazo wanazipitia, waweze kumruhusu Mungu awe karibu nao ili aweze kuwatendea vile ambavyo ni Mungu tu ndiye anayeweza kuwafanyia.**



*Dayosisi ya Barisal, Bangladesh*

# MUNGU ANAYESEMA

## Ufunuo 1:10-11

*Nalikuwa katika Roho, siku ya Bwana,nikasikia sauti kuu nyuma yangu, kama sauti ya baragumu ikisema, 'Haya uyaonayo uyaandike katika kitabu, ukayapeleke kwa hayo makanisa saba...'*

Mahali popote tarumbeta ikipigwa, watu wanakuwa makini. Iwe ni tarumbeta ya pembe inayotumika huko Uganda inayoitwa eng'ombe, au tarumbeta ya shaba inayopulizwa katika sherehe za harusi huko India, au tarumbeta ya Moari ya kukaribisha wageni iitwayo Pūkāea. Katika tamaduni zingine ikiwemo watu wa Dinka huko Sudan Kusini, ngoma ndio huwa zinatumika katika jukumu hilo. Hautakiwi kupuuzia unaposikia sauti yake. Inaweza kuwa inatoa onyo, kusherehekea tukio la furaha, kukaribisha ugeni, au sauti ya kujiandaa na vita; kamwe hupaswi kupuuzia sauti hiyo.

Yohana alipokuwa mafichoni huko Patmos, akiwa ametengana na marafiki zake, kanisa na familia yake, bila shaka alijiuliza ni huduma gani ambayo bado anaweza kuifanya, ghafla utulivu uliokuwepo katika ibada yake ya Jumapili ukavunjwa na sauti kuu; sauti ya Bwana Yesu. Yule yule Yesu ambaye alikuwa mwokozi wake na rafiki yake, akimhakikishia mtume kwamba, kazi yake bado haijakamilika, kuna huduma mpya ya kufanya.

Matokeo ya yeye kusikiliza ni kitabu cha Ufunuo ambacho katika mistari ya mwanzoni kinasema 'Mungu huwabariki wale wasikiao ujumbe na kutii.' Katika sehemu zingine duniani, hilo ni kinyume na tamaduni zao. Kama inavyosemwa katika Masomo ya Biblia ya Kiafrika: 'Katika sehemu nyingi, Wakristo wanadhihakiwa, na Biblia inadharauliwa.'

Tarmbeta ya kwenye Biblia, ambayo shahidi wa Mageuzi, Askofu mkuu Cranmer,



*Kongamano la Ufufuo, Jimbo la Trinidad na Tobago*

aliipa jina 'Neno la Mungu lililoandikwa', haikomi kulia. Lakini, ingawa kamwe haiwezi kunyamazishwa, tunaweza kuacha kuisikiliza. Ni rahisi sana kuona kwamba tumesongwa na mambo mengi ya kufanya na kushindwa kutenga muda kila siku kusoma Biblia na kumuomba Roho Mtakatifu atumie neno hilo maishani mwetu. Mambo haya mengine mara nyingi ni mazuri – michezo, shughuli na watoto, kukaa na marafiki, na masaa mengi ya kufanya kazi na kukaa na familia – lakini hatuchukui muda na kuuweka kwa ajili ya Neno la Mungu.

Kwenye baadhi ya tamaduni, wanaotuzunguka wanatutaka tuchukue kisu na kukata sehemu zetu wasizozipenda: sehemu ambazo zinapingana dhambi na ubinafsi. Tunatakiwa kuyatanguliza Maandiko mbele ya tamaduni zetu. Kwa mfano, tamaduni zinaposukuma kulipa kisasi na kudai kuwa 'dawa ya moto ni moto au jicho kwa jicho na jino kwa jino', tunatakiwa kuwafundisha kuwa neno la Mungu linasema hatutakiwi kulipa kisasi bali tuipishe ghadhabu ya Mungu, kwani yeye anasema kuwa 'Kisasi ni juu yangu mimi' (Warumi 12:19). Ukweli kuhusu kisasi ni kwamba husababisha mzunguko unaojirudia wa kisasi. Mahatma Gandhi ananukuliwa akisema, 'Jicho kwa jicho watu dunia nzima vipofu'.

---

**Tunapoendelea kuomba kwa ajili ya marafiki zetu watano leo, omba wao na sisi pamoja, tusikie neno la Mungu kwa uwazi na ufasaha. Kama Askofu mkuu Cranmer alivyosema 'Chochote kilichopatikana, kinapaswa kuchukuliwa kama cha msingi na ukweli usiokuwa na makosa.'**

---

# MUNGU ANAYEUMBA

Ufunuo 1:8

*'Mimi ni Alfa na Omega', asema Bwana Mungu, aliyeko na aliyekuwako na atakayekuja, Mwenyezi.*

Mstari huu mfupi mwanzoni mwa kitabu cha mwisho cha Biblia unazungumza mengi sana kuhusu Mungu. Huyu ni Mungu aliyeumba kila kitu, anayejifunua, na kutuokoa kupitia Bwana Yesu Kristo na kukaa katika maisha ya kila amwaminiye Yesu kama Roho Mtakatifu.

Agano Jipya liliandikwa kwa lugha ya Kigiriki. Herufi ya kwanza na ya mwisho katika lugha ya Kigiriki ni, Alfa na Omega, ambazo zimetumika hapa kumwelezea Mungu, hii iliwahakikishia Wakristo waliokuwa wakikabiliana na mateso ya Warumi kwamba, chochote kinachowatokea, Mungu yupo nao na wako salama wakati huo na milele.

Tukirejea katika kitabu cha kwanza cha Biblia, yaani kitabu cha Mwanzo, tunaona Mungu akiumba kila kitu, ikiwa ni pamoja na mwanadamu ambaye aliumbwa kwa sura yake. Anawapa jukumu la kuitunza bustani aliyoiumba. Hii inatukumbusha kwamba Mungu wetu ni Mwenyezi. Ni rahisi kwa imani yetu kuwa tu kama mti mmoja uliojitenga katika pori la maisha yetu badala ya kumruhusu Mungu Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, kuwa msingi wetu, kutupatia nguvu, na kuwa nyumba yetu ya kudumu.

Mungu anapenda kuumba na kutengeneza upya pale vitu vinapoharibika. Pale hili linapotokea, pale dhambi zetu zinapoharibu na kuweka jeraha katika ulimwengu, katika uhusiano wetu na wengine na uhusiano wetu na Mungu, tayari kuna wokovu ameuweka kwa ajili yetu. Wokovu huo ndio uliopelekea kifo cha msalaba, ufufuo na utukufu wa mbinguni kwa wote wanaomwamini mwana wake, Yesu Kristo.



*Ofisi ya Kanisa la Anglikana*

Usemi fulani wa Kiafrika unasema: 'Ukitaka kukaa kivulini utakapokuwa mzee panda mti hivi sasa.' Mwenyezi Mungu, anataka tukae naye milele katika kivuli cha mbingu aliyoiumba amepanda mti kwa mfano wa Yesu pale msalabani. Kwa msaada wa Roho wake Mtakatifu sisi sote sasa ni viumbe wapya, na kitu anachokitamani ni kila mtu ashiriki katika hilo na wengine.

Matamanio ya watu wengi kwa sasa duniani kote ya kuitunza dunia yetu ni mfano wa maana ya kuumbwa kwa sura ya Mungu. Tunatamani kuwa wakulima wa bustani hata kama hatumjui Bwana wa bustani hiyo.

---

**Tunapoendelea kuwaweka watu wetu watano mbele za Bwana, mshukuru Mungu kwa ajili yao na uombe matamanio yao na yetu pamoja ya kutunza uumbaji wa Mungu yatatupelekea kumjua na kumpenda yule aliyeviumba.**

---

# MUNGU ANAYETOA

## Ufunuo 3:7-8

*Haya ndiyo anenayo yeye aliye mtakatifu, aliye wa kweli, aliye na ufunguo wa Daudi, yeye mwenye kufungua wala hapana afungaye, naye afunga wala hapana afunguaye: 'Nayajua matendo yako. Tazama, nimekupa mlango uliofunguliwa mbele yako, ambao hapana awezaye kuufunga.'*

'Zawadi za bure!' ni moja ya ahadi kubwa ya matangazo mengi. Hata kama ni kitu ambacho haukihitaji wala haukitaki, wazo la kwamba ni bure mara nyingi linatuvuta. Katika historia, watu wengi wametoa ahadi za upendeleo wa Mungu ikiwa tu mwombaji atatoa dhabihu fulani, atafanya jambo fulani au atasafiri na kwenda sehemu fulani inayosemekana kuwa ni 'takatifu'.

Habari Njema ya Kikristo ni tofauti na ya kustaajabisha kabisa. Moja ya mstari unayopendwa sana katika Biblia, unapatikana katika Injili ya Yohana 3:16 nao unasema, 'Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.' Mungu hutoa tena na tena. Sisi kama Wakristo, tunatakiwa kupokea zawadi hii ya bure. Tumepewa uzima wa milele katika Yesu Kristo, na hatujafanya jambo lolote ili kustahili kuupata. Tunaweza kupumzika huku tukifahamu kwamba haijalishi kile tunachofanya, lakini Mungu tayari ameshafanya.

Mstari wa leo kutoka katika Ufunuo unatoka katika ujumbe wa kanisa lililopo katika mji wa Philadelphia ilipo Uturuki leo. Palikuwa ni kitovu kikubwa cha biashara, mahali ambapo kununua na kuuza bidhaa ilikuwa ni maisha ya kila siku. Yesu anaandika kwamba atawapa zawadi nyingine bure. Anawahakikishia kwamba wanaweza kupumzika kwake. Kamwe hatawapa kitu cha kuwadhuru, bali atawapa zawadi ambayo itakua na kulikuza kanisa…

Anawapa mlango ulio wazi!



*Tukio la Lugha Tatu la Ufalme Wako Uje, Colombo, Sri Lanka*

Je, hiyo inaonekana kuwa zawadi ya ajabu? Inawezekana wao wangependelea zaidi kama maombi yao yangejibiwa, zawadi zaidi za kiroho, uwepo wake wa karibu, au mambo mengine mengi. Walichokipata ni waliambiwa kumshirikisha Kristo na marafiki zao, jamii zao, na miji yao.

Ufalme Wako Uje kwa urahisi maana yake ni kuomba 'Roho Mtakatifu Aje' katika maisha ya watu tunaowafahamu, labda watu watano tu, ili kwamba watokee kufahamu upendo unaookoa wa Mungu kupitia Bwana Yesu. Kristo anatuambia kwamba amefungua mlango, tunachotakiwa kufanya ni kupita katika mlango huo.

Kila wakati tunapozungumza au kutenda matendo kwa wanaotuzunguka huku upendo wa Mungu ukiwa ndani ya mioyo yetu, basi hapo tunakuwa tunapita katika mlango ambao Yesu aliufungua.

Wakati mwingine tunahisi kwamba juhudi zetu ni ndogo na hazileti matokeo yoyote. Kuna usemi wa Kiafrika unaochekesha utakaotufundisha. Unasema, 'Ukidhani wewe ni mdogo sana kuweza kufanya mabadiliko, jaribu kukesha usiku na mbu.' Msemo huu ni wa kweli kwangu kwa wiki hii ninapoandika nikiwa Juba hapa Sudan Kusini, ambapo kuna mbu wengi.

---

**Unapoendelea kuwaombea marafiki zako watano, muombe Mungu afungue milango mingi zaidi kwa ajili yako ili uweze kusambaza neno la Mungu kwa watu wengine ili waweze kumfahamu Bwana Yesu Kristo.**

---

# MUNGU ANAYETEMBEA NA SISI

## Ufunuo 1:12-16

*Nikageuka niione ile sauti iliyosema nami. Na nilipogeuka, niliona vinara vya taa saba vya dhahabu, na katikati ya vile vinara nikaona mtu mfano wa Mwanadamu, amevaa vazi lililofika miguuni, na kufungwa mshipi wa dhahabu kifuani.Kichwa chake na nywele zake zilikuwa nyeupe kama sufu nyeupe, kama theluji; na macho yake kama mwali wa moto,na miguu yake kama shaba iliyosuguliwa sana, kana kwamba imesafishwa katika tanuru; na sauti yake kama sauti ya maji mengi. Naye alikuwa na nyota saba katika mkono wake wa kuume; na upanga mkali, wenye makali kuwili, ukitoka katika kinywa chake; na uso wake kama jua liking'aa kwa nguvu zake.*

'Je, kweli ni wewe?' Huwa tunauliza hivyo tunapokutana na mtu ambaye hatujaonana naye kwa miaka kadhaa. Kuna namna wanakuwa wanaonekana tofauti. Anakuwa amevaa mavazi tofauti, inawezekana labda anakuwa amepungua au kuongezeka, labda anakuwa amebadilisha mtindo wa nywele, lakini siku zote kunakuwa na kitu kinachowafanya tuwatambue kwamba hakika ni wao.

Hata hivyo, kwa Yohana, hakuwa na shaka kwamba aliyekuwa akizungumza naye alikuwa ni Yesu, yeye ambaye amefika mpaka mafichoni kwake, katika kumbukumbu zake, katika upweke wake, katika imani na matumaini yake. Kuna mengi sana ambayo ni ya tofauti katika umbo hili la ajabu ambalo analiona. Picha za Agano la Kale zinamjia akilini mwake huku mtu huyu anapozidi kuonekana vizuri zaidi.

Vazi refu na mshipi wa dhahabu kifuani unaleta taswira ya vazi analovaa Askofu Mkuu akimwonyesha Yesu aliyetufia katika Ijumaa Kuu ya kwanza, na yeye aliye Mwana wa Kondoo wa kweli wa Mungu ambaye huchukua dhambi za ulimwengu.

Nywele zake nyeupe na moto ni taswira ya Mungu Mwenyezi kutoka katika kitabu cha Danieli sura ya 7. Hakika yeye anayezungumza anazungumza kwa mamlaka ya Bwana wa vitu vyote. Bila shaka, lugha iliyotumika katika Danieli 7 imekuwepo



*Watoto katika Shule ya Anglikana Fiji*

tangu mwanzo wa somo la leo katika usemi wa 'Mmoja aliye mfano wa mwanadamu'. Yohana anamuona Bwana aliyeshinda katika Agano la Kale ambaye pia ni rafiki yake katika Injili. Mwana wa Adamu ndivyo Yesu alivyojizungumzia mara nyingi.

Hebu fikiria: Unaangalia huku na huko baada ya kusikia sauti ya Mungu na unamuona rafiki yako wa karibu akikutazama. Rafiki ambaye alitembea pamoja na wewe kando ya Ziwa Galilaya na katika mitaa yote ya Yerusalemu. Rafiki ambaye alijua kusherehekea katika sherehe za harusi katika kijiji cha kana na rafiki ambaye aliwaona wanafunzi wake wote wakikimbia kwa hofu katika bustani ya Gethsemane. Rafiki huyu ana miguu ya 'kama iliyosuguliwa na moto'. Kauli hiyo inazungumzia utu wa Yesu kama vile sehemu nyingine iliyobaki inavyoashiria Uungu wake.

Rafiki huyo huyo wa Yohana anataka kuwa rafiki yetu pia. Anataka kutembea pamoja nasi. Mwana wa Mungu ambaye alizaliwa kwenye zizi, ambaye alikimbia kama mkimbizi, aliyefanya kazi ya ufundi seremala; yeye aliyewapenda wenyeukoma, aliyekula chakula na wakusanya kodi, na aliyekuwa rafiki na makahaba na kuwalisha wenye njaa.

Yesu huyu huyu anaendelea kutupa mkono wake ili tuwe marafiki zake.

---

**Omba kwamba watu wako watano watamfahamu zaidi Yesu ambaye hakika anafahamu hali zetu zilivyo.**

---

# MUNGU ANAYESIKILIZA

## Ufunuo 2:9

*'Naijua dhiki yako na umaskini wako, lakini u tajiri.'*

Ni jambo la kipekee sana pale mtoto wako anapokwambia kichekesho chake cha kwanza. Inawezekana akawa amekisikia shuleni au amekuwa akikifanyia mazoezi mara kwa mara kichwani mwake mpaka muda atakapofika nyumbani ili akiseme mbele ya familia nzima! Anakuwa anacheka kila wakati akikisema. Familia yake inacheka pia...ingawa wameshakisikia hapo awali. Japokuwa wameshasikia tayari haiwazuii kusikiliza kwa makini na kuipokea kama vile ndio wanasikia kwa mara ya kwanza. Hii yote ni ili kujenga uhusiano.

Tunaposali, aidha tunajiombea wenyewe, au tunaombea marafiki zetu au tunaombea masuala makubwa ya kitaifa – kama njaa, vita, hali ya hewa, au umasikini – sio kwamba tunamwambia Mungu mambo ambayo hayafahamu. Hatuwezi kumshtukiza na jambo jipya lakini yeye anapenda kuwa na uhusiano nasi na tunapofanya mazungumzo tunajikuta akili zetu, mioyo yetu na matamanio yetu yanakuwa yanaendana na upendo na mipango ya Mungu.

Ilikuwa hivyo kwa kanisa la Smirna katika mstari wa leo. Waliishi katika mji mzuri sana, lakini uzuri wake ulifunikwa na ibada za sanamu na kuwatesa Wakristo. Sanamu hizo kwa leo zinaweza kuchukua umbo tofauti – mawazo ya kisiasa, mambo ambayo watu maarufu wanapenda, shinikizo kwa rika lako – lakini kutesa Wakristo kwa leo kumetawala zaidi kuliko wakati wowote katika historia.

Hivyo basi tunapomshirikisha Bwana tabu zetu tunamshirikisha matatizo yetu, tulipokwama na hofu zetu kama walivyofanya kaka na dada zetu karne kadhaa duniani kote.

Tunachogundua ni kwamba Bwana anatukumbusha kuhusu utajiri wetu.

Mamlaka kuu haipo mikononi mwa majeshi au wanasiasa; ipo mikononi mwa Baba yetu wa mbinguni ambaye kamwe huwa hasahau. Yeye ni Baba anayejua kila kitu kuhusu sisi na baba ambaye, ikiwa tutamwamini Yesu, atatupitisha katika lolote ambalo litakuja mbele yetu na kisha kutukaribisha katika uzima wa milele mbinguni.

Hii ilikuwa ni kweli kwa Wakristo wa Smirna miaka elfu mbili iliyopita na pia ni kweli kwetu hivi sasa. Pamoja na kuwaombea watu wako watano leo, watangulize mbele za Mungu watu wanaoteswa kwa sababu ya imani yao kwa Yesu ambao siku moja tutakutana nao katika utukufu. Tukumbuke kwamba Mungu anaelewa walichokipitia, na tuendelee kusimama kwa uhakika tukifahamu kwamba yeye anafahamu yote tunayoyapitia. Bwana anasikia maombi yetu, na anayajibu yote kwa kusema 'ndiyo', 'hapana' au 'subiri'.

Tunapomwambia kuhusu shaka zetu na jinsi tunavyozitambua dhambi zetu, yeye anatukumbusha kwamba Yesu ndiye njia, ya ukweli na uzima, na kwamba msamaha wake ni bure na kamili. Tunapomwambia kwamba tunajihisi hatuna nguvu, yeye anatukumbusha kuhusu nguvu ya Roho Mtakatifu.

---

**Tunapowaleta marafiki zetu watano kwake na kumwambia kwamba hatujui namna ya kumshirikisha Yesu kwao, anatukumbusha kwamba aliahidi kutupa maneno na kwamba hakuna mahubiri makubwa zaidi ya kuishi maisha ya Kristo.**



*Askofu wa Rutana & mke wake wakiwa Jimbo la Rutana, Burundi*

# MUNGU ANAYEOKOA

Ufunuo 1:17-18

*Nami nilipomwona, nalianguka miguuni pake kama mtu aliyekufa. Akaweka mkono wake wa kuume juu yangu, akisema, 'Usiogope, Mimi ni wa kwanza na wa mwisho, na aliye hai; nami nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele. Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu.'*

Kuna hadithi fulani kuhusu wachimba madini wawili wa Afrika Kusini. Mmoja wao alikuwa Mkristo na mwingine alikuwa haamini kwamba kuna Mungu. Walipokuwa wakiendelea kuchimba makaa ya mawe pamoja, kipande cha jiwe kilichomoka na kumdondokea yule aliyekuwa haamini uwepo wa Mungu kichwani kwenye kofia. Alipata woga akidhani kwamba sehemu yote ya juu ingeporomoka na kuwafunika alilia kwa sauti akisema 'Ee Mungu nisaidie!'. Rafiki yake Mkristo alitabasamu na kumjibu: 'Unaona, nilikwambia, hakika jiwe la kaa la mawe linatosha kuondoa hali ya kutoamini kutoka kwa mtu.'

Kuna nyakati katika maisha yetu tunapitia na zinatufanya tusimame na kutafakari maswali makubwa yaliyopo maishani mwetu. Je, haya yote yanamaanisha nini? Je, Mungu kweli yupo? Je, kweli mbingu ipo, na kama ipo, kweli nina uhakika kama nitakwenda huko? Maono ya Yohana ya Yesu Kristo katika utukufu wake, yalimshtua, kumshangaza na pia kumrejeshea nguvu.

Alichofanya ni 'kuanguka miguuni mwake kama vile nilikuwa mfu'. Ilikuwa ni kama vile Isaya alichokifanya, alipoelezea katika Isaya 6: 'Kisha nikasema, "Ole wangu! Nimepotea, mimi ni mwenye dhambi."'

Kiuhalisia binadamu anapokutana na uwepo wa Bwana wetu mtakatifu anagundua kwamba Yeye ni mtakatifu sana na sisi siyo watakatifu.

Maisha ya Bwana Yesu yalikuwa ya ukamilifu. Tunasoma katika Injili na



*Wajumbe wa Kongamano la Lambeth*

tunafahamu kwamba huyu tunayekutana nae ni wa kipekee na wa tofauti sana na yeyote yule. Yeye ni uzima tunaouhitaji kuishi.

Tunapogundua kwamba sisi ndio wale ambao Biblia inawaida wenye dhambi, watu wale ambao hawawezi kufikia viwango vya Mungu, haitakiwi kutuhusunisha na kuwa mwisho wetu kama binadamu; bali tunatakiwa kuitumia hii kama hatua mojawapo katika kufahamu kwamba Mungu ana mpango wa kutukomboa. Mpango huo ni Yesu; anatupa nafasi ya kuchagua mpango wake wa kutuokoa.

Majibu ya Mungu kwa mahitaji yetu ni msamaha wa bure na kamili, kama ilivyokuwa kwa Isaya katika Agano la Kale na kwa Yohana katika Agano Jipya. Isaya anabeba taswira ya mkaa wa kusafishia na Yohana ana mkono wa uponyaji wa Bwana Yesu wa kumrejesha. Kumbuka hadithi ya Mwana Mpotevu. Aliandaa hotuba yake vizuri alipokuwa katika banda la nguruwe; lakini anafika na kumwona baba yake akimkimbilia na kumpa mavazi, pete, na viatu na kumkaribisha kwa sherehe.

Kuna msemo mmoja wa Kiafrika unaosema, 'Yule anayesamehe, ndiye mshindi!' Bwana Yesu, ambaye pale msalabani, aliomba kwa ajili ya wanajeshi waliomsulubisha, ni mshindi mkuu na tunapompokea kama Bwana wetu tunashiriki nae katika ushindi huo.

---

**Omba kwa ajili ya wale unaowaweka mbele za Mungu wafahamu furaha ya kukaribishwa kwenye karamu ya milele na kupumzika katika msamaha wa Yesu.**

---

# MUNGU ANAYETUPA CHANGAMOTO

## Ufunuo 2:4-5

*Lakini nina neno juu yako, ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza. [5] Basi, kumbuka ni wapi ulikoanguka; ukatubu, ukayafanye matendo ya kwanza. Lakini, usipofanya hivyo, naja kwako, nami nitakiondoa kinara chako katika mahali pake, usipotubu.*

Waraka wa Bwana kwa kanisa katika Efeso unaweza kuwa ni wenye nguvu zaidi kuliko yote ambayo Yohana aliandika. Hili lilikuwa ni kanisa lake. Anawaandikia nyumbani kwake, na japokuwa Yesu anasifu utakatifu wa Kanisa na kazi ngumu inayofanyika ya kusambaza Habari Njema, kuna changamoto moja kubwa. Uwepo wa kanisa upo hatarini, isipokuwa tu mpaka pale watakapoutambua tena upendo wa kweli wa Kikristo kwa Bwana na kwa watu wengine.

Upendo wa miaka iliyopita hauna faida tena leo.

Ikiwa upendo wa Mungu umebadilishwa na kuwa tabia za mazoea tu, na kama upendo wa waumini wenzetu kanisani umegeuzwa kuwa na urasimu na kukalishwa vikao visivyokuwa na mwisho, basi ule moto umezima. Hatari iliyopo ni kwamba tutageuka kuwa ganda tupu tu bila chochote ndani yetu.

Masomo ya Kiafrika ya Biblia yanasema hivi: 'Hakuna mtu anayependa kula chakula kilichochacha au kusoma gazeti la miaka ishirini iliyopita. Tunataka chakula safi na habari za sasa. Basi tusimpe Mungu upendo uliochacha na baridi. Tufanye toba dhidi ya kujifanyisha ndani ya kanisa.' Sio ajabu kwamba barua za Yohana zimejaa maneno ya kuhimiza jamii ya Kikristo kupendana. Ilifika wakati, alipokuwa na umri mkubwa sana Yohana bado aliwahimiza waumini 'Watoto wadogo pendaneni', mstari huu unaonekana kuwa na maana zaidi katika ulimwengu wa leo.

Yesu ametupa changamoto, pamoja na kututia moyo, kama kanisa. Pale Biblia



*Wamawake wakisali katika Jimbo la Barisal Diocese, Bangladesh*

inapotoa changamoto kwetu: jambo tunalotakiwa kulibadilisha, jambo la kulifanyia kazi, kitu fulani ndani yetu kilicho kwa namna ambayo hakitakiwi kuwa, ni rahisi sana kusema kwamba, 'Nimekata tama, sina nguvu ya kufanya chochote kuhusu hilo. Nimejaribu na kushindwa mara nyingi sana.' Hicho sio kitu Mungu anachotaka. Na ndiyo maana ametupa nguvu ya ajabu ya Roho Mtakatifu ili aweze kufanya kile ambacho hatuwezi kukifanya.

Kama Bwana Yesu angetuandikia barua wewe na mimi ni jambo gani ambalo angetuandikia ili kututia moyo? Ni mabadiliko gani, kwa neema yake, tayari yamekwishafanyika? Katika maombi yetu ya leo, tumuombe atuonyeshe, maeneo ya maisha yetu ambayo anataka kuona mabadiliko zaidi, kasha muombe nguvu ya Roho Mtakatifu kufanya mabadiliko hayo yawezekane.

Mchoraji anapochora picha ya mtu, kwanza anaanza kwa kuchora mistari ya haraka au mistari ya mwanzo ya kumuongoza kasha anaongezea juu yake mistari na rangi nzuri mpaka picha kamili inapokamilika. Sisi tunapaswa kuwa kama picha, picha ya Kristo kwa ulimwengu, hivyo tunaomba mchoraji mtakatifu yeye atuchore kwa muonekano wake. Maneno ya wimbo huu wa zamani uitwao Bwana Ning'arishe, Bwana anatukumbusha kuishi kwa namna ambayo itawawezesha watu kumuona Kristo kupitia sisi: *'Ning'arishe Bwana, ning'arishe Bwana, katika yote niyasemayo au kuyafanya; ili ulimwengu uone kuwa Kristo anaishi ndani yangu, na kujifunza kumpenda pia.'*

**Omba kwamba watu wetu watano waweze kumuona Bwana Yesu katika maisha ya watu wake.**

# MUNGU ANAYEWEWEZESHA

## Ufunuo 3:20-22

*'Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami. [21] Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi. [22] Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa.'*

Hivi hauvutiwi na mistari ya kupendeza kama hii? Ni miongoni mwa mistari ya thamani zaidi kwa Wakristo wengi duniani katika Agani Jipya. Moja ya mchoro maarufu sana wa Kristo uliofanywa na msanii kutoka Victoria kwa jina la William Holman Hunt, unamuonyesha Kristo akibisha hodi nje ya mlango ambao hauna kitasa kwa nje na unaweza kufunguliwa kutokea ndani tu. Anasema kwamba alichora mchoro huo, '...kwa kile alichokiona kama ni amri takatifu, na sio tu kama mchoro mzuri.'

Katika mistari hii Bwana Yesu anawaandikia Wakristo wa Laodikea ambao walijiona kuwa wametajirika kiroho, kuliko watu wengine, na kwamba hawahitaji chochote. Aliwafanya watambue kwamba walikuwa ni, 'masikini, vipofu na walio uchi'; na kwamba wafungue milango ya kanisa lao na milango ya mioyo yao, ili Kristo awafikishe pale walipotakiwa kuwa.

Laodikea ilifahamika kwa nguo zake za thamani, madawa yake ya kutibu macho na utajiri wake; hata hivyo hatujaitwa kuangalia vitu vya kidunia.

Tumeitwa ili kuwa kama Bwana Yesu. Hatupaswi kutambulishwa kwa uraia wetu, utajiri au umasikini wetu, elimu yetu au kazi yetu bali kwa utu wetu, 'ndani ya Kristo', kama alivyosema Mtakatifu Paulo.

Kumkaribisha Kristo aishi katika maisha yetu sio tu pale unapoamua kuokoka, japo ni 'mabadiliko makubwa' ambayo ishara yake kuu ni ubatizo. Ni muhimu kuishi na Kristo kila siku, haijalishi umekuwa Mkristo kwa muda mrefu kiasi gani.

Kuna msemo wa Kiafrika unaosema, 'Mtumbwi kamwe sio mkubwa sana kiasi kwamba ushindwe kupinduka na kuzama.' Kuna wakati ambapo kiburi chetu, tamaa yetu ya kujitegemea, inaingia kati na kutuzuia kufanana na Bwana Yesu. Kamwe hatuwezi kuwa wakubwa sana, wazee sana, tuliokomaa sana, wenye akili sana, muhimu sana kiasi kwamba tusihitaji kuongozwa na Kristo.

---

**Omba kwamba watu wako watano pia wawe wanyenyekevu kumsikia Kristo akibisha hodi na kuwaita mlangoni mwa maisha yao na wafungue mlango na kumkaribisha Yesu kwani anasubiri wamkaribishe.**

**Kama vile wale wanafunzi walipokuwa njiani kuelekea Emau katika Luka 24, tunagundua kwamba tunapomfungulia Kristo mlango, anakuwa si mgeni tena bali mwenyeji. Msisahau kuwafadhili wageni, maana kwa njia hii wengine wamewakaribisha malaika pasipo kujua (Waebrania 13:2).**



*Mchungaji Bob Key na Viongozi kutoka Korea Kusini*

# PENTEKOSTE

## ‘Roho Mtakatifu Uje’

Ufunuo 3:22

*‘Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa.’*

Kuna msemo wa Kiafrika unaosema, ‘Kusikiliza ni ujuzi mgumu zaidi kujifunza na muhimu sana kuwa nao.’ Mwisho wa barua zote kwa makanisa saba mwanzoni mwa Ufunuo inasema ‘Kila mwenye sikio la kusikia na asikie neno la Roho na afahau kwamba anayaambia makanisa.’ Ujumbe kwa kila kanisa ni tofauti lakini amri ya kusikiliza na kuelewa kile Roho anachokisema ni muhimu kwa wote.

Tumewaombea watu wetu watano, wanaopendwa na Mungu. Tumeombea makanisa yetu na tumeomba sisi binafsi ‘Roho Mtakatifu Uje’ katika kipindi hiki chote cha Ufalme Wako Uje. Sasa siku ya Pentekoste imefika, ni wakati mzuri wa kuuliza, ‘Je, Roho Mtakatifu anataka mimi nisikie nini, nikielewe, kukiweka ndani moyo wangu na kukifanyia kazi?’

Bwana Yesu alipoandika kwa makanisa ya Ufunuo kupitia Yohana, aliandika akifahamu fika hali iliyopo, matumaini yao, hofu, ndoto, changamoto, makosa na udhaifu wa kila kanisa na kila muumini. Barua hizo zilitokana na upendo mtakatifu unaotamani Wakristo wote wapate faraja wanapokuwa katika dhiki, nguvu na fursa wanapokuwa katika udhaifu.

Bwana Mungu anatamani makanisa, pamoja na sisi, tufike pale tunapotakiwa kuwa, kupitia nguvu za Roho Mtakatifu.

Siku ya kwanza ya Pentekoste, ambayo Luka anaifafanua katika Matendo ya Mitume sura ya pili, wanafunzi ambao kama sisi tu, walikuwa wakiomba tangu



*Ibada katika Kanisa la Mtakatifu John huko Hong Kong*

siku ya Kupaa kwa Kristo, walipokea zaidi ya vile walivyofikiria. Upepo wa Roho uliwabeba na kuwapeleka katika mitaa ya Yerusalemu ili kusambaza Habari Njema kuhusu kifo na ufufuo wa Bwana Yesu. Moto wa Roho ulianza kuwabadilisha kuanzia ndani yao na kuwapa zawadi na kuwawezesha kufanya mambo mapya na kushinda majaribu ya zamani. Lugha waliyopewa na Roho ilikuwa ni ishara ya kwamba Yesu alikuwa ni kwa ajili ya ulimwengu mzima.

Ulimwengu wetu unahitaji lugha tofauti na zile zilizotumiwa katika siku ya kwanza ya Pentekoste. Kuna mahitaji mapya, tamaduni mpya, vizazi vipya vya kufikiwa, lakini Injili ya Yesu kamwe haiwezi kubadilika. Alikufa kwa sababu ya dhambi mara moja. Akafufuka. Atarudi tena kama Bwanana hakimu.

Kama ilivyokuwa kwa wanafunzi wa kwanza, tunaishi katika kipindi cha kabla ya ujio wa pili wa Kristo. Tunaishi na amri hiyo moja masikioni mwetu, 'Enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi' (Mathayo 28:19). Tunasonga mbele kwa ujasiri tukifahamu kwamba tunawezeshwa na Roho Wake. Tunafanya hivi tukikumbushwa na usemi kwamba tunasambaza neno la Mungu kwa nguvu ya Roho Mtakatifu na tunamwachia Mungu matokeo.

**'Bwana, wasaidie watu wangu watano wasikie Wito wako, wajibu upendo wako na kumkubali Bwana Yesu. Amina'**



thykingdomcome.global